OFISI YA RAIS.
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA

SHULE YA SEKONDARI MLOWA,

S. L.P 1197,

IRINGA.

13/12/2021

Kumb.Na MLSS/JOINING/2021/001

JINA LA MWANAFUNZI_____

_____

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MLOWA MWAKA 2021

1.0 UTANGULIZI

Ninayo furaha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Mlowa mwaka 2021. Shule ipo umbali wa kilomita moja toka stand ya mabasi ya Ndorobo (**Mlowa**). Shule ni ya kutwa na ina hosteli kwa wanafunzi wasichana. **Ili kupata nafasi ya kuishi hosteli lazima iombe kwa kamati ya uendeshaji wa hosteli na kupewa form ya taratibu za hostel (kwa wanafunzi wasichana tu)**
Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 11/1/2021.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 SARE ZA SHULE

WASICHANA

A. Sketi mbili (2) rangi ya kijani ndefu.
B. Brauzi mbili rangi nyeupe mikono mifupi.
C. Viatu jozi mbili rangi nyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba vyenye kisigino kifupi.
D. Soksi jozi mbili rangi nyeupe.
E. Raba za michezo
F. Nguo za michezo (track za michezo rangi ya kijani kibichi)
G. Vazi la hijabu kwa wanafunzi wa waislamu lifanane na sare ya shule.

WAVULANA

A. Suruali mbili (2) rangi ya kijani iwe na mifuko mitatu, mkunjo wa chini (turn up) marinda mawili (celebration) na iwe na upana unaoridhisha chini zisiwe zinazobana mwili (model).
B. Mashati mawili (2) rangi nyeupe mikono mifup.
C. Viatu jozi mbili rangi nyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba vyenye kisigino kifupi.
D. Soksi jozi mbili rangi nyeusi au kahawia.
E. Raba za michezo
F. Nguo za michezo (bukta, t shirt, track za michezo rangi ya kijani kibichi)

2.2 MAAGIZO MENGINE

A. Daftari kubwa 10 kwa ajili ya nukuu za masomo na daftari ndogo kumi za kufanyia mazoezi.
B. Flat file moja kwa ajili ya kutunzia Kumbukumbu zake.
C. Viandikio; kalamu za wino za kutosha, kalamu za mkao na vifutio.
D. Mkebe wa vifaa vya mahesabu na kuchorea na rula.
E. Vifaa vya usafi binafsi ndoo moja ukubwa itakayotumika kutunzia Maji kwani Maji hayapatikani muda wote.
F. Aje na jembe moja lenye mpini.
G. Mahitaji ya usafi binafsi na afya kwa wanafunzi wasichana.
H. Tochi moja ya betri mbili au ya umeme wa jua atakayotumia kukiwa na tatizo la umeme.

3:0. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknologia na Ufundi, yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Rais TAMISEMI yenye jukumu la kusimamia na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yaliyoainishwa katika form hii

- Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ni lazima.
- Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni.
- Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazoelekezwa.
- Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.

SHERIA ZA SHULE

Tabia njema ni ya lazima na inatiliwa mkazo hapa shuleni. Mwanafunzi mwenye tabia mbaya hafai kupewa elimu ya sekondari au hata elimu ya juu. Ni lazima mwanafunzi awe na tabia nzuri na kufuata taratibu za shule pia kuwatii walimu na wafanyakazi wengine.

MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

A. Wizi, uasherati, ubakaji na ushoga, ulevi na matumizi mabaya ya madawa ya kulevya, uvutaji wa bangi na sigara.
B. Makosa ya jinai kadiri ya sheria za nchi mfano kupigana.
C. Kuharibu mali kwa makusudi, kudharau bendera ya Taifa.
D. Kuoa au kuolewa kupata mimba au kusababisha mimba ndani au nje ya shule.
E. Kugoma, kuchochea na kuongoza matendo ambayo yanavuruga amani na usalama wa watu mfano kuitisha vikao visivyo rasmi.
F. Kukataa adhabu kwa makusudi, kutohudhuria masomo darasani kwa mujibu wa sheria.

Hakuna msamaha wowote utakao tolewa baada ya mwanafunzi kutenda makosa haya

SHERIA KWA UJUMLA

A. Kunywa pombe, kuvuta sigara/madawa ya kulevya au kiko ni mwiko.
B. Uasherati wa aina yoyote ni kosa kubwa sana na hauruhusiwi shuleni.
C. Kila mwanafunzi ni lazima awe mtiifu kwa walimu wake wote, wafanyakazi wote viranja wote wa shule, na wakuu wengine wote. Ujeuri na ubishi wa aina yoyote ni mwiko mwanafunzi anatakiwa aheshimu kazi za mikono zote.
D. Matusi ya aina yoyote, yawe ya kusemwa au kuandika hayaruhusiwi shuleni.
E. Kila mwanafunzi lazima aheshimu na kutunza mali za shule.Uharibifu wowote utakao tokea itabidi ugharimiwe na mwanafunzi mwenyewe.
F. Sare za shule (uniform) ni lazima zivaliwe wakati wote wa masomo.
G. Wizi wowote hauruhusiwi shuleni, iwe ni mali ya shule au mali ya mwanafunzi au mfanyakazi.
H. Usafi wa mwili, mavazi na wa madarasa ni wajibu wa kila mwanafunzi.
I. Ugomvi wa aina yoyote au kupigana na kurushiana maneno mabaya ni mwiko shuleni. Kuchelewa kwa aina yoyote ni kosa.
J. Tabia njema shuleni na nje ya shule ni wajibu na ni lazima kwa kila mwanafunzi.
K. Taa za shule na mali za shule ni lazima vitumiwa kwa uangalifu.
L. Magazeti au vitabu vyenye picha au maneno yasiyofaa havitakiwi shuleni.
M. Upokeaji au uandishi wa maneno yasiyofaa ni mwiko shuleni.
N. Uhusiano wa mwanafunzi wa kike na wa kiume uwe ni wa kimasomo tu na si vinginevyo aidha uwe ni ule wa kaka na dada.
O. Unapaswa kufahamu mipaka ya shule na kutotoka bila ruhusa.
P. Mwanafunzi haruhusiwi kwenda nyumbani kwa mwalimu au mfanyakazi yoyote isipokuwa inapolazimu kwa ruhusa maalumu. Maeneo hayo ni nje ya mipaka ya shule.
Q. Si ruhusa kutoka katika eneo la shule wakati wa masomo bila ruhusa. Hairuhusiwi kugoma, kusababisha mgomo hapa shuleni.
R. Mwanafunzi hairuhusiwi kuwa na mimba, kutoa mimba au kusababisha mimba kwa wenzake au kwa mtu mwingine yeyote.
S. Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na dawa hosteli kama anazo anapaswa kukabidhi kwa mwalimu wa afya na kuendelea kuzitumia kwa kadri ya maelekezo ya matabibu.
T. Mwanafunzi haruhusiwi kuuza mali yake au kununua mali ya mwanafunzi mwingine.
U. Mwanafunzi haruhusiwi kupita njia zisizo rasmi bila ruhusa maalumu.

MATIBABU

Wagonjwa wote watapata matibabu kwenye Kituo cha Afya MLOWA. Ikishindikana kupata huduma ya matibabu yanayohitajika, basi muuguzi ataishauri ofisi ya malezi/ mwalimu wa zamu ambaye ataandika ruhusa ya kwenda kutibiwa hospitali ya wilaya. **MWANAFUNZI AJE NA BIMA YA AFYA**

MATUMIZI NA UTUNZAJI WA MALI YA SHULE

A. Kila mwanafunzi anatakiwa kutumia na kutunza vizuri mazingira, mali za shule kama vile majengo, viti, meza, madawati, majembe, vitabu, vitanda ndoo na vifaa vyote vya shule
B. Hakikisha taa zote zimezimwa wakati wa mchana na kufunga mabomba ya maji ukiyakuta yako wazi.

C. Weka mazingira ya shule kuwa safi na kuvutia kwa kutunza miti, kuokota karatasi na uchafu wowote. Pita kwenye njia za miguu kama unavyuoelekezwa na sheria za shule. Usikatishe katika viunga na kukanyaga maua na majani yalioteshwa.

MAWASILIANO

Mawasiliano ya ana kwa ana kati ya mzazi na uongozi wa shule ni muhimu sana kwa maendeleo ya mwanafunzi. Kama litatokea tatizo lolote linalomuhusu mwanao kimasomo au kitabia ni vizuri mzazi awasiliane na uongozi wa shule mara moja. Pia shule itawasiliana mzazi/mlezi mara moja endapo itatokea lazima ya kufanya hiyo**.**

NI MARUFUKU MWANAFUNZI KUMILIKI SIMU YA MKONONI AKIWA HAPA SHULENI.

"ELIMU NI NGUZO YA MAISHA".

.....

Frank Mahai

MKUU WA SHULE

1. Viambatisho na Fomu Muhimu:

a) Fomu ya uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali.

b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makossa ya jinai.

c) Mkataba wa mwanafunzi, mlezi/mzazi baina ya shule ya sekondari ifunda.

d) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sharia, kanuni kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

e) Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

2. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

Nakala

1. Katibu Mkuu,
Ofisi ya Rais,TAMISEMI
S.L.P. 1923, **DODOMA.**

2. Mkurugenzi wa Elimu ya Sekondari,
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
S.L.P. 9121, **DAR ES SALAAM**.

3. Afisa Elimu (M),
S.L.P. 858, **IRINGA.**

4. Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Iringa,
S.L.P. 108, **IRINGA.**

5. Afisa Elimu Sekondari (W),
S.L.P. 642, **IRINGA**.

JAZA FOMU HIZO NA KUZIRUDISHA SHULENI WAKATI WA KURIPOTI

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA

Sehemu ya Mwanafunzi:

Mimi. ..... Msichana/Mvulana ninakubali nafasi niliyopewa kuingia kidato cha ..... mwaka ..... katika Shule ya Sekondari ya Mlowa, na nitafika shuleni bila kuchelewa. Nitatii na kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zote za shule na za Nchi.

Nitakuwa Mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kazi za Elimu ya Kujitegemea.

Sehemu ya Mzazi/Mlezi

Mimi. .....Ninakubali mtoto wangu kuingia Shule ya Sekondari Mlowa kidato cha ..... mwaka .....na

Ninaahidi kumpatia mahitaji yote kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na Shule (Joining Instructions) ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na Shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa Shule na Taifa.

Anwani yangu ya kudumu ni:

.....

.....

.....

Namba ya simu ya mkononi ..... ya mezani/ofisini.....

Iwapo nitapata uhamisho au kubadilisha makazi ni lazima nitaijulisha shule kwa maandishi yaliyothibitishwa na Mkuu wangu wa Idara au Ofisi ya Afisa Mtendaji wa Kata/Kijiji.

Sahihi ..... Tarehe .....

SHULE YA SEKONDARI YA MLOWA
S.L.P. 1197
IRINGA

TAARIFA YA BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. Jina …….....tarehe ya kuzaliwa…….....

(taja mwaka na mwezi)

2. Kabila …….....Taifa …….....

3. Dini …….....

4. Jina la Baba …….....

5. Anwani ya Baba …….....

…….....

6. Kazi ya Baba …….....

7. Jina la Mama …….....Kazi yake …….....

8. Wazazi wanaishi pamoja au wametengana…….....

9. Jina na anwani ya Mlezi wako (kama si Mzazi) …….....

…….....

10. Wakati wa likizo utakwenda kwa nani na wapi …….....

(taja sehemu moja tu utakakokwenda kila wakati).....

Endapo una ndugu jaza jedwali lifuatalo hapa chini.

JINA LAKE	UHUSIANO	MAHALI ANAPOISHI	ANWANI NA NAMBA YA SIMU

11. Ninathibitisha kwamba habari zote nilizotoa ni kweli na sahihi

Sahihi ya Mwanafunzi……..... Tarehe: ……

Sahihi ya Mzazi/Mlezi ……..... Tarehe ……

12. Jina na sahihi ya Afisa Mtendaji wa Kijiji …….....

Mhuri: .....

AHADI YA MWANAFUNZI, MZAZI /MLEZI KWA
SHULE YA SEKONDARI MLOWA

Mimi.....Mwanafunzi wa Kidato cha..... Mwaka 20…

Ninaahidi:

1. Kufuata sheria na taratibu zote za shule kama zilivyoainishwa katika Fomu ya maelekezo ya Kujiunga na Shule hii niliyojaza hapa shuleni.
2. Kuhudhuria vipindi vyote Darasani kwa kuzingatia ratiba ya shule. Kwenda kinyume na sheria hii nichukuliwe hatua za kinidhamu.
3. Kuzingatia Taaluma kwa kuweka juhudi ili kufaulu masomo vizuri.
4. Kutunza na kulinda miundo mbinu yote ya shule. Kuharibu miundo mbinu hiyo nitalazimika kulipa gharama na kuitengeneza; mifano ya miundo mbinu bomba,rangi za kuta ,miundo mbinu ya umeme, vioo, madirisha, taa, dari, milango na vitasa, miundo mbinu ya vyoo, n.k.

5. Kutunza vifaa vya maabara na vitabu vya shule. Kuvunja , kuharibu na kupoteza vifaa au vitabu nitalazimika kulipa kifaa au kitabu husika.

6. Kutunza samani zote za shule. Kuharibu samani za shule nitalipa samani au gharama husika.

7. Kuja na Kamusi ya Kiingereza kwa ajili ya matumizi yangu binafsi- Advanced Oxford English Dictionary (O Level Students Only).

8. Kutumia lugha ya kiingereza wakati wote nitakapokuwa shuleni.

9. Kukabidhi namba za Mzazi / Mlezi kwa utawala kwa ajili ya mawasiliano muhimu. Na kuwasiliana na namba nitakazopewa na uongozi wa shule. Endapo nitatumia njia tofauti nitapewa adhabu kali.

10. Sitajihusisha na mapenzi au kuwa na mahuasiano ya kimapenzi na mwanafunzi mwenzangu au mtu yeyote ndani au nje ya shule. Ikibainika nichukuliwe hatua za kinidhamu.

11. Kuwepo bwenini kwa wakati sahihi, kulala bwenini katika chumba nilichopangwa kila siku. Kwenda kinyume na utaratibu huu nichukuliwe hatua za kinidhamu.

12. Kuzingatia tarehe ya kufunga shule na kufungua shule kwa kutoondoka mapema kabla ya shule kufungwa na kuripoti shule tarehe ya kufungua shule. Kwenda kinyume na hili ninakosa sifa yakuendelea kusoma katika shule hii, hivyo nifukuzwe shule.

Jina la Mwanafunzi. .....Saini..... Tarehe.....

Mzazi/Mlezi

Mimi..... Nimesoma na kuelewa yaliyoandikwa ninakubaliana na Masharti haya ambayo ni nguzo muhimu kwa ufaulu na maendeleo ya mwanangu kwa faida binafsi na Taifa kwa ujumla. Hivyo nitamwezesha mwanangu kwa hali na mali kuweza kukamilisha hayo ili kuweza kufaulu Kitaaluma.

Anwani yangu ya kudumu.

.....

.....

.....

Namba ya simu. ..... ya mkononi/Mezani /Ofisini…….

Nakubali haya mbele ya:-

PRESIDENT'S OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENTS

IRINGA DISTRICT COUNCIL

MLOWA SECONDARY SCHOOL

FORM MEDICAL EXAMINATION

(To be completed by a Medial Officer in respect of all Form I entrants)

Pupil's full name…….....

Age ……..... (years) Sex …….....

Blood count (Red and white) …….....

Stool Examination …….…….....

Syphilis and other venereal diseases test …….....

……..…….....

T.B. Test ……..…….....

Eye Test …….....

Ears ……..…….....

Spleen ……..…….....

Abdomen …….....

Urine for plamotest …….....

Test for pregnancy (for girls only) …….....

ADDITIONAL INFORMATION

(If any) e.g. physical defects, impartments e.g. am legrete)

Infections, chronic of family diseases etc …….....

……

……

I certify that the above is fit/not fit to pursue studies in Secondary Education.

Station…… Signature …….

Date ……. Designation ……